*Mulika, Na. 43 (2), 321-335*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Mla: Kiunzi cha Uzingatizi wa Maadili ya Waswahili katika Methali Teule za Kiswahili

*Martina Duwe*[1]
Chuo Kikuu Mzumbe

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na43t2.7

**Ikisiri**

Thamani ya Mla hubainika kupitia mahangaiko ya kusaka mlo utakaomfaa yeye na jamii yake kwa jumla. Katika mahangaiko hayo, Mla huweza kutenda kinyume na maadili yanayopaswa kuzingatiwa na jamii yake. Matendo hayo huweza kumwathiri yeye au/na jamii inayomzunguka. Kwa kuzingatia hilo, methali za Kiswahili zimesukwa kwa ufundi unaobainisha namna Mla anavyoweza kuzingatia maadili kulingana na maisha halisi ya Waswahili. Hata hivyo, haiko bayana ni kwa namna gani methali zenye kufungamanishwa na neno 'mla' zinavyobeba umahususi wa uzingatizi wa maadili kwa Mla. Kwa msingi huo, makala haya yanafafanua namna methali zenye kumrejelea Mla zinavyobeba na kudokeza maarifa mbalimbali ya kimaadili kulingana na kaida za jamii. Ili kufanikisha hilo, ilitumika mbinu ya uchambuzi matini ambapo methali zenye kuhusishwa na neno 'mla' zinazotumiwa na Waswahili zilisaidia katika kupata data za matokeo haya. Vilevile, katika makala haya, imetumika Nadharia ya Uhalisia kama mwegamo mkuu katika kuchunguza, kuchanganua na kuwasilisha data husika. Matokeo yanaonesha kuwa dhana ya mla katika methali za Waswahili haijatumika kimakosa, bali imelenga kusisitiza na kuhifadhi maarifa mbalimbali ya kimaadili yanayotosheleza utamaduni wao. Kwa hiyo, makala haya yanajadili kwa kina vipengele vya maadili vinavyosisitizwa kwa Mla kupitia methali teule za Kiswahili. Vipengele hivyo vya kimaadili ni: kuthamini na kuheshimu udugu, kutambua tabia za watu, kuthamini wakati wa sasa, kuwajibika na kujituma katika kufanya kazi, kutambua athari za kupokea hisani na kutambua athari za wema na ubaya.

## 1.0 Utangulizi

Fasili ya msingi ya dhana Mla hurejelea mtu anayependelea kula vyakula vya aina fulani (BAKITA, 2017). Kifasihi, neno hili hutumika kwa kuhusianisha na maneno mengine katika ujenzi wa methali za Kiswahili zenye kuibua na kubainisha maarifa ya kimaadili. Maarifa hayo husawiri kaida za Waswahili wenyewe katika kulinda na kuenzi ustawi wa maisha yao (Senkoro, 1988). Kwa kuzingatia hilo, Mla katika makala haya inafafanuliwa kama istiara inayorejelea mtu mwenye nafasi au mafanikio fulani, mathalani, ya kiuongozi, kiuchumi, kielimu na kisiasa.

[1] **Baruapepe:** magriccola@gmail.com

Mjadala unamakinikia dhana hii kwa kuhusianisha na hali ya mtu ya mafanikio katika nyanja mbalimbali za maisha yake. Hali ya kuwa na mafanikio huweza kumtofautisha Mla na wengine katika muktadha wa tabia, mwonekano na thamani anayopewa kutoka kwa wanaomzunguka kama kielelezo cha maadili, ambapo fasihi ya Kiswahili inabainisha jambo hilo. Fasihi ya Waswahili hutumika kutoa mafunzo ya kimaadili yanayosawiri tamaduni za jamii ya Waswahili wenyewe (Bertoncini, 1989). Methali, kama kipera kimojawapo cha fasihi ya Kiswahili, ni nguzo muhimu katika kubainisha na kuhifadhi maarifa ya kimaadili yanayozingatiwa na Waswahili. Methali hizo hupewa maana kulingana na muktadha wa kijamii, kihistoria na kusudi la kuwasilisha ujumbe husika na athari yake hubainika kupitia mwitiko wa wapokezi (Mulokozi, 2017). Kwa msingi huo, methali inaweza kuwa na maana zaidi ya moja kulingana na kusudi, muktadha na wakati wa uwasilishwaji wake. Naye Okpewho (1992) anaeleza kwamba katika maisha ya Waafrika, methali ni utungo wenye thamani na kutumika kwake hutegemeana na maadili yanayolengwa kusisitizwa na kurithishwa kulingana na utamaduni wao. Kwa msingi huo, msuko wa methali za Kiswahili hujiegemeza katika maana inayolengwa kufika kwa mpokezi ambapo maneno huteuliwa na kupangwa kulingana na utoshelevu wa kimaana. Jambo hili husawiri utamaduni wa matumizi ya lugha ya kibunifu yenye mpangilio wa tamathali za semi, sitiari, nidaa, taswira na mbinu nyingine za matumizi ya lugha ili kufunza maadili fulani ya jamii (Simiyu, 2011; Mlaga, 2017). Hivyo basi, dhana ya mla hufungamanishwa katika tungo za fasihi, hasa methali, ili kuwasilisha maadili hayo kwa hadhira ya Waswahili wenyewe kulingana na umilisi wa maana zinazosawiri utamaduni wao.

Kila jamii inaongozwa na misingi fulani ya kimaadili kulingana na utoshelevu wa kaida zake. Maadili ni mwenendo mzima wa tabia ifaayo katika kuendesha maisha ya kundi la watu fulani (Bergner, 2010; Udokang, 2014). Mwenendo huo hujipambanua kupitia matendo mbalimbali ayatendayo Mla ambayo hudhihirisha thamani na utu wake kulingana na tamaduni za jamii yake halisi. Baadhi ya matendo hayo ni: uvaaji, uongeaji, heshima, utiifu na unyenyekevu, mshikamano, upendo, uvumilivu na kujitoa kwa ajili ya wengine (Duwe, 2024). Kila jamii hujengwa kwa misingi ya kimaadili yenye kuzingatia imani fulani katika kuendesha maisha yake. Kwa Waafrika, hususani Waswahili, huamini na kusisitiza suala la mwenendo mwema kwa kila mtu kama msingi wa kuishi kwa amani na upendo kupitia sanaa yao, kimahususi methali zinazowakilisha utamaduni wao (Miruka, 2005). Kwa hiyo, kila mwanajamii hupaswa kuishi kwa kujikita katika misingi ya maadili hayo.

Waswahili ni watu wote wanaozungumza Kiswahili katika sehemu mbalimbali ndani na nje ya Afrika Mashariki (Senkoro, 1988; Madumulla, 2009). Wataalamu hawa wanaendelea kueleza kwamba Waswahili licha ya kupatikana kwa wingi Afrika Mashariki; pia, wameenea katika maeneo mengi ulimwenguni kote. Hata

hivyo, waliopo nje ya Afrika Mashariki wanachukuliwa kwamba maarifa na ujuzi wa kutumia lugha ya Kiswahili wamevipata Afrika Mashariki au kwa watu kutoka Afrika Mashariki waliopo maeneo mengine ulimwenguni. Kwa ujumla, wataalamu hawa wanayakinisha kuwa Waswahili ni watu wote wanaotumia lugha ya Kiswahili na kuuishi utamduni wake bila kujali maeneo wanamopatikana. Wataalamu wengine wanaeleza kwamba Waswahili ni watu wenye asili ya mwambao wa Afrika Mashariki na visiwa vyake (Sengo na Kiango, 1973; Mulokozi, 2017). Hii inatokana na ukweli kwamba watu waishio katika mwambao wa Afrika Mashariki wanatumia Kiswahili kama lugha kuu ya mawasiliano na sehemu ya utamaduni wao. Kwa kuzingatia mitazamo hii miwili ya fasili kuhusu Waswahili, makala haya yanawatazama Waswahili kuwa ni watu wanaopatikana ndani au nje ya Afrika Mashariki ambao wanauishi utamaduni wa Waswahili.

Katika kushughulikia dhana ya mla, makala yameongozwa na swali la msingi ambalo ni ‘kwa nini Mla arejelewe kwa namna tofauti katika methali za Kiswahili?’ Kwanza, jambo lolote duniani linakamilishwa na Mla. Matendo yake yanaweza kuleta athari chanya au hasi kulingana na utamaduni wao. Pili, mahangaiko ya Mla hutokana na hitaji la msingi katika kulinda uhai na ustawi wake, ambalo ni kula. Mla hufanya kazi mbalimbali ili apate mlo utakaomwezesha kuishi na kustawi vema duniani (Hart, 2019). Mahangaiko hayo yanaweza kumfanya atumie njia ambazo ni kinyume na matakwa ya jamii yake. Methali hizi zinamkumbusha Mla kuhusu ukengeufu wa kimaadili katika kulinda na kuhifadhi historia yake. Hii ni kutokana na ukweli kwamba Mla anaweza kuwa na tabia mpya ambayo ni kinyume na maadili ya jamii yake. Kwa msingi huo, dhana hii huchopekwa katika maneno mengine na kuunda methali za Kiswahili ili kusisitiza, kuonya au kurekebisha mienendo ya Mla katika jitihada za kujipatia mlo. Jitihada hizo zinaweza kutumia mipango na matendo ambayo ni kinyume na matakwa ya jamii yake. Hivyo, methali hizo hubainisha maadili ya msingi yanayopaswa kuzingatiwa na Mla kama kiunzi cha uzingatizi wa maadili katika jamii yake.

## 2.0 Mwegamo wa Nadharia

Misingi ya Nadharia ya Uhalisia imetumika katika kuchunguza, kuchanganua na kuwasilisha matokeo ya utafiti uliolenga kuchunguza maadili yanayosisitizwa kwa Mla kupitia methali za Kiswahili zenye dhana ya mla. Westphal (1989) na Wamitila (2022) wanaeleza kwamba katika muktadha wa sanaa, misingi ya nadharia hii imetokana na fikra za mwanafalsafa wa Kiyunani Hegel aliyeumulika na kuufafanua ulimwengu kama duara halisi la ukamilifu wa mwanadamu. Aliitazama sanaa na yote yanayobuniwa na mwanadamu kama akiso la utoshelevu wa fikra na maisha yanayofungamana na utamaduni wake. Mawazo yake yaliendelea kutumiwa na wataalamu mbalimbali katika kuhakiki kazi za kisanaa. Msingi mkuu wa nadharia hii unajikita katika kuonesha namna kazi za sanaa zinavyosawiri ulimwengu kama ulivyo na siyo kama unavyotarajiwa kuwa (Larkin, 1977). Dhana hii ilianza kutumiwa na wanafasihi karne ya kumi na tisa

katika mchakato wa kupinga tapo la uromansia lililokuwapo kabla yake ambalo halikuyabainisha mambo kama yanavyoonekana kwenye jamii (Mulokozi, 2017). Wanauhalisia walilenga kuyamulika na kuyaelezea maisha kama yalivyo au yanavyotendeka katika jamii bila kuweka vionjo vya kiulimbwende. Nao Wafula na Njogu (2007) na Ogechi (2024) wanaeleza kwamba watafiti na wahakiki wanaojiegemeza katika mtazamo huu wachunguze na kufafanua jambo kama linavyotokea katika mazingira halisi ya mwanadamu. Kwa kuzingatia hilo, data za matokeo haya zimepatikana kutokana na mtafiti kujiegemeza katika msingi unaodai kuwa fasihi ni akiso la mazingira halisi ya jamii. Hivyo, mtafiti alichunguza uhalisi wa vipengele vinavyobainisha maadili yanayosisitizwa kwa Mla kama kiunzi cha uzingatizi wa maadili hayo. Vilevile, uchambuzi na uwasilishaji wa data hizo umejikita katika kubainisha namna methali teule zinavyousawiri utoshelevu wa maadili kulingana na kaida halisi za Waswahili.

## 3.0 Methodolojia

Uchunguzi na uchakataji wa matokeo ya makala haya umezingatia mkabala wa kitaamuli. Data za matokeo haya zilikusanywa maktabani kwa kudurusu matini mbili zenye mkusanyiko wa methali za Kiswahili. Matini hizo ni *Kamusi ya Methali* (2018) na *Dira ya Methali:Kitabu cha Marejeleo* (2022). Katika matini hizi, methali zilizomakinikiwa ni zile zenye kufungamanishwa na dhana ya mla kama kiunzi cha usukaji wa methali hizo. Methali tisa (9) ziliteuliwa na kutumika kama sampuli katika mjadala huu ili kuthibitisha msisitizo wa maadili ya Waswahili kwa Mla. Methali hizo zilipatikana kwa mbinu ya usampulishaji lengwa wa kipekee kwa kuteua zile zinazoambatana na neno ‘mla’ pekee. Uteuzi wa methali hizi umezingatia kwamba dhana ya mla inayorejelewa katika methali nyingi za Kiswahili inadokeza msisitizo wa maadili kwa Mla ambaye hutenda yote yanayobainika katika ulimwengu wake. Aidha, Mla ndiye mwenye dhamana ya kulinda na kuhifadhi maadili yanayosawiri jamii yake kupitia vitu anayovihangaikia na vile vilivyohangaikiwa au kutafutwa na wengine. Maadili mbalimbali hubainishwa kupitia methali za Kiswahili ili kuakisi mwenendo wa kimaadili aufanyao Mla katika jamii yake. Methali hizi zimetumika kama sampuli ili kubainisha maadili hayo. Kwa jumla, uwasilishaji wa matokeo yaliyopatikana ulihusisha data za utafiti, taarifa mbalimbali za kitafiti, pamoja na Nadharia ya Uhalisia.

## 4.0 Vipengele vya Maadili Vinavyosisitizwa kwa Mla kupitia Methali Teule za Kiswahili

Matokeo yanaonesha kwamba Waswahili hulifungamanisha neno ‘mla’ katika maneno mengine na kuunda tungo ya kibunifu, hususani methali, ili kufunza maadili mbalimbali yanayosawiri utamaduni wao. Kwa hiyo, makala haya yanajadili vipengele sita vya maadili yanayosisitizwa kwa Mla kupitia methali teule za Kiswahili ambavyo ni: kuthamini na kuheshimu udugu, kutambua tabia za

watu, kuthamini wakati wa sasa, kuwajibika na kujituma katika kufanya kazi, kutambua athari za kupokea hisani na kutambua athari za wema na ubaya.

**4.1 Kuthamini na Kuheshimu Udugu**

Maisha ya Waswahili yamekitwa katika misingi ya kuthamini na kuheshimu ndugu. Udugu ni uhusiano kutokana na uzawa wenye asili moja na hujumuisha familia pamoja na ukoo (Widmer, 2006). Kwa Waswahili, ndugu hujumuisha jamii pana inayoweza kumulikwa kwa namna mbili: kwanza, wale waliotokana na baba na mama mmoja; pili, udugu ambao hujumuisha kundi la watu waliotokana na kiini au asili moja ya ukoo, mathalani, bibi na babu, baba mkubwa au mdogo, mama mkubwa au mdogo, mjomba, shangazi na binamu. Sambamba na hao, ndugu anaweza kuwa mtu yeyote, mathalani, jirani au rafiki anayekuthamini na kukujali. Pia, mtu huyo hujulikana kama *ndugu wa hiyari*. Umuhimu wake maishani ndio unaowaunganisha na kuchukuliana kama ndugu. Naye Udokang (2014) anaeleza kwamba ndugu, kwa Waafrika, si lazima wazaliwe tumbo moja bali hutazamwa katika misingi ya kujaliana na kuthaminiana. Kwa msingi huo, ndugu hujumuisha mlolongo wa wanaomzunguka Mla katika mazingira yake halisi. Hata hivyo, Waswahili huamini kwamba ndugu wa kweli atakayeambatana na Mla katika nyakati zote anazopitia ni yule wa uzao mmoja. Haya yanabainika kupitia sanaa yao, ikiwamo methali zao za Kiswahili ambapo Mla anasisitizwa kuheshimu, kuthamini na kujali ndugu. Mfano wa methali hizo ni “Mla nawe siye mfa nawe, bali mzaliwa nawe”.

Kiuhalisi, Mla akiwa na mali au mafanikio fulani maishani mwake watu hujitokeza ili wale naye mali hizo. Watamsifia, watamheshimu na kumjali katika kipindi hicho ili waendelee kufaidika kutoka kwake. Mali hizo zitakapokwisha au akipata shida fulani, taratibu wataanza kukaa mbali naye. Watu wenye nasaba naye ndio watakaokuwa na uchungu naye katika wakati huo mgumu anaoupitia. Dhana ya mla katika methali hii huwakilisha mtu ambaye ananufaika kwa Mla kutokana na mafaniko yake. Hivyo, ‘Mla nawe siye mfa nawe’ humaanisha kuwa wanaonufaika kutoka kwako sio watakaokuwa nawe wakati wa maumivu au mateso yako. Mathalani, mtu anapofilisika kiuchumi marafiki na wale waliokuwa karibu naye humtenga kwa kuwa hawapati chochote tena kutoka kwake. Pia,‘bali mzaliwa nawe’ humaanisha kwamba ndugu watabaki pamoja nawe katika hali yoyote utakayopitia. Maishani, Mla anakumbushwa kuwathamini na kujenga mahusianao mazuri na ndugu kama hazina ya maisha ya baadaye. Matokeo yanaonesha kwamba wakati wa shida Mla anaweza kukimbiwa na marafiki aliokula nao na watakaobaki naye ni ndugu zake wa kuzaliwa pamoja. Hii ni kutokana na ukweli kwamba hana faida tena kwao na wakati mwingine hukwepa jukumu la kumhudumia au kumsaidia katika shida aliyonayo. Zaidi, Hart (2019) anaeleza kwamba ili uijue tabia halisi ya mtu anayekuthamini angalia uwajibikaji wake wakati unapokuwa na uhitaji wa kuhudumiwa au kusaidiwa naye. Katika maisha ya Waswahili, ni halisi kwamba mafanikio huibua tabia mpya ya

mwanadamu ambapo huweza kuchukuliwa na kutazamwa kwa namna tofauti katika jamii yake. Kwa msingi huo, mafanikio humbainisha Mla kama ni mwema au si mwema, mtulivu au mwenye papara ya maisha, na mwenye kuthamini na kujali ndugu au la.

Kimsingi, maadili kuhusu heshima, utiifu, na unyenyekevu kwa ndugu na wakubwa wengine katika maisha ya Waswahili husisitizwa kwa kiwango kinachohifadhi na kulinda utamaduni wao kama jamii mojawapo inayopatikana Afrika. Methali hii inasisitiza kuwajali na kuwaheshimu ndugu katika nyakati zote. Waswahili hutumia methali hii endapo kuna viashiria vya kudharau au kutoheshimu ndugu ili kukemea tabia hiyo. Kwa kujiegemeza katika mtazamo wa Wanauhalisia unaosisitiza kwamba sanaa ni akiso la maisha halisi ya jamii, ni dhahiri kwamba katika maisha ya Waswahili, wala na Mla ni wengi lakini wasitiri wa Mla ni wachache. Haya yanashadidiwa vema na Agozino (2018) kwamba kuheshimu na kuwajali ndugu ni hazina ya baadaye, hasa wakati wa shida kama wahenga wasemavyo, ‘mcheza kwao hutuzwa’. Utu wa mtu kwa Waswahili hupimwa pia kwa kigezo cha kuthamini na kujali ndugu ambapo huanzia katika ngazi ya familia. Hivyo, methali hii inaikumbusha jamii ya Waswahili kwamba kutomthamini ndugu ni kitendo kimojawapo cha ukengeufu wa misingi ya kimaadili.

### 4.2 Kutambua Tabia za Watu

Tabia ni jumla ya mwenendo au matendo fulani ya mwanadamu ambayo hutendwa kwa kurudiwarudiwa na huchukuliwa kama nyenzo ya utambulisho wake katika jamii (Bergner, 2010). Mtaalamu huyu anaendelea kueleza kwamba tabia ni mwitiko wa kifikra unaofungamana na kuchochewa na malezi ya jamii yanayokitwa katika misingi ya kimaadili asilia. Kila mwanadamu ana tabia inayombainisha na kumtambulisha kwa upekee wake katika jamii inayomzunguka (Duwe, 2023). Waswahili katika kuishi kwao, humtazama mtu kulingana na mwonekano na tabia yake. Hata hivyo, ni vigumu kubaini tabia ya mtu na kumhukumu kulingana na anavyoonekana. Matokeo yanaonesha kwamba kuna watu ambao kwa mwonekano wa nje ni tofauti na ukweli walioubeba mioyoni mwao. Huonekana kama wazuri, wema na waadilifu. Kiuhalisi, ndani yao, yaani kifikra na kivitendo ni wabaya katika jamii. Haya yanaelezwa zaidi na Gencer (2019) kwamba tabia ya Mla ipo ndani na kubainika kwake ni kupitia matendo ayafanyayo. Mathalani, anaweza kuwa mpole kwa kumtazama sura yake, anasaidia watu na anaongea kwa busara lakini kiuhalisi ndiye mtenda maovu kuliko wengine. Fasihi ya Waswahili, hususani methali, hasa zenye kuambatana na neno Mla, hudokeza maarifa ya kutomwamini Mla kwa kuutazama mwonekano wake wa nje. Mfano wa methali hiyo ni “Simba mwenda pole, ndiye Mla nyama”.

Methali hii inatoa tahadhari katika suala la kumwamini Mla kutokana na mwonekano wake. Kiuhalisi, simba anapokuwa mawindoni huwa mpole na

mwenye kutumia akili ili aweze kupata mnyama amtakaye. Kirai 'simba mwenda pole' katika methali hii kimetumika kama istiara inayomaanisha mwanadamu anayeonekana mzuri au mwema kwa wanaomzunguka ili kupata kitu fulani. Ni vigumu kumbaini mtu mwenye tabia hii hadi atakapoonesha viashiria fulani na, wakati mwingine, haoneshi tabia yoyote ila athari yake itabainika baadaye. Kuishi na watu kunahitaji umakini utokanao na mafunzo yanayotolewa katika jamii kupitia sanaa kama vile methali ili kuepukana na watu wabaya. Pia, 'ndiye mla nyama' ni istiara yenye maana kwamba ndiye anayetenda maovu katika jamii. Kwa kuongozwa na fikra za wanauhalisia kwamba kazi ya kisanaa husawiri maisha ya jamii, ni kanuni ya maisha ya Waswahili kwamba Mla hapaswi kuhukumu kuwa mtu fulani ni mzuri au mwema kwa kuona kuwa ni mpole kupitia sura na sauti yake. Ndani yake anaweza kuwa mwenye tabia mbaya inayoweza kuleta maangamizo katika jamii. Hoja hii inafafanuliwa vema na Kamugisha (2020) anayesema kwamba, maishani, ni vigumu kuyaelewa mawazo na fikra za mwanadamu hadi yanapobainika dhahiri kwa wanamzunguka kupitia matendo yake. Kwa kuzingatia hilo, ni vema kuishi kwa tahadhari na kuwa na tabia ya kuwachunguza watu kwa muda mrefu ili kujua usahihi wa tabia zao.

### 4.3 Kuthamini Wakati wa Sasa

Wakati hukamilishwa na Mla ambaye huutumia katika kutafuta mlo wake. Wakati wa sasa kwa Waswahili una thamani zaidi ikilinganishwa na wakati uliopita au ujao. Hii ni kwa kuwa wakati wa sasa ndio unajibainisha kwa matendo ambayo yanaweza kuonekana na kuthibitishwa kwa kuona, kusikia hata kutenda (Prior, 1967). Mla katika mahangaiko yake ya kusaka kula huumulika wakati wa sasa ambao humtambulisha na kumthaminisha kwa wanaomzunguka. Hivyo, jamii humpa thamani kutokana na kile anachokipata sasa kama asemavyo Calhoun (2018) kwamba mwanadamu huutazama wakati wa sasa kwa thamani kubwa kuliko wakati uliopita kwa kuwa ndio wakati anaouishi na unaobainisha nafasi yake kwa jamii inayomzunguka. Waswahili, kama sampuli ya jamii zilizopo Afrika, hutumia methali mbalimbali zinazoambatana na neno Mla ili kuthibitisha kwamba anayekula leo ni wa thamani zaidi kuliko aliyekula jana. Mfano mzuri wa matheli hiyo ni "Mla, mla leo, mla jana kala nini?"

Kifungu cha methali hii kisemacho 'Mla, mla leo' kinamaanisha kwamba mwenye thamani ni yule anayekula, anayepata mafanikio fulani au anayetenda sasa. Waswahili kulingana na kaida zao, sasa ndiyo inayobainisha uwezo na jitihada za Mla katika kufanya yote yanayoonekana ndani ya jamii yake. Kwa hiyo, thamani yake hutokana na anavyoonekana kwa wakati wa sasa. Pia, 'Mla jana kala nini' katika methali hii humaanisha kwamba jana haina thamani kwa kuwa imeshapita. Hivyo, aliyepata, aliyetenda au kufanikiwa jana, thamani yake hailinganishwi na anayepata au kufanikiwa leo. Mathalani, kiongozi aliyeko madarakani, kwa Waswahili, hupewa thamani zaidi kuliko yule aliyeng'atuka au kutolewa. Thamani hiyo hutokana na ukweli kwamba kiongozi wa sasa ndiye mtawala, yaani Mla;

hivyo, walio chini yake humthamini kwa kuwa kula kwao kunategemea maamuzi yake. Kwa kuzingatia mawazo ya wanauhalisia kwamba fasihi ni akiso la maisha ya jamii, ni wazi kuwa mtazamo wa Waswahili kuthamini wakati wa sasa kuliko uliopita katika shughuli za kiuchumi na kijamii unasawiri misingi halisi ya utamaduni wao. Haya yanaelezwa vema na Prior (1967) na Kijogoo (2021) kuwa mwanadamu, katika ulimwengu wake, huuthamini wakati wa sasa kwa kuwa huutumia katika kuzalisha na kuongeza kipato kinachompa thamani.

Kwa Waswahili, kama sampuli mojawapo inayopatikana Afrika, wakati uliopita ni historia inayomsaidia Mla kuutumia wakati wa sasa katika kutafuta mlo. Kadhalika, maisha yenye maana na thamani ni yale ya duniani, si yale ya baada ya kufa ambayo si maisha bali ni hali ya kuwapo tu kama asemavyo Mbiti (2011) kwamba, thamani ya mwanadamu ni wakati wa uhai wake. Kwa mantiki hiyo, baada ya kifo thamani yake ni ya kidhahania na kihistoria inayotokana na kukumbukwa kwa yale aliyoyatenda wakati wa uhai wake. Hivyo, kuendelea kuishi kwake ni suala la kiimani kulingana na tamaduni za Waafrika. Kimsingi, methali hii inabainisha mtazamo wa Waswahili kama wasemavyo wahenga kuwa leo ni leo asemaye kesho ni mwongo; kwamba yanayotendeka leo huthaminiwa kuliko wakati uliopita. Hivyo, kupitia methali hii Mla anahimizwa kuutumia vema wakati wa sasa ili kuweza kujitosheleza na kustawisha maisha yake ya leo na baadaye.

### 4.4 Kuwajibika na Kujituma katika Kufanya Kazi

Kuwajibika na kujituma katika maisha ya Waswahili ni suala linalohimizwa na kuzingatiwa katika jamii yao. Maarifa ya msingi yanayosisitizwa kwa jamii ni kufanya kazi kwa bidii ili kuongeza uzalishaji mali utakaostawisha familia, kaya na taifa kwa jumla. Hivyo, kila mmoja anahimizwa kuwajibika kulingana na mgawanyo wao wa kimajukumu. Haya yanaelezwa vema na Calhoun (2018) anayesema kuwa ulimwenguni, thamani ya mtu katika jamii yake hutokana na kazi anayoifanya kwa bidii. Juhudi hizo zinaweza zikamfanya awe na kipato tofauti na wengine ambao watalazimika kumpa heshima ya kiwango cha pekee. Anaendelea kueleza kwamba uvivu na uzembe humdunisha mtu katika jamii yake kwa kuwa hataweza kuongeza kipato kinachosaidia kuendesha maisha ya jamii; hivyo, hudharaulika. Kwa msingi huo, mchango wa mtu katika jamii yake hutazamwa na hupimwa kulingana na uwajibikaji wake katika shughuli mbalimbali za kiuchumi, kiutamaduni na kijamii. Kimsingi, kufanya kazi ni mchakato unaoambatana na maumivu, mateso, uchungu, kujinyima na uvumilivu. Hatimaye, mafanikio ni matokeo ya ushindi wa maumivu na machungu hayo. Katika kueneza maadili haya, kuna methali ambazo hudokeza kwamba Mla anayewajibika kusaka riziki yake kwa taabu, atakula kwa furaha. Methali ifuatayo ni mfano wa hizo, “Mla cha uchungu, na tamu hakosi.”

Methali hii inasisitiza kwamba, anayewajibika katika shughuli mbalimbali ndiye anayefanikiwa. Uwajibikaji katika maisha ya mwanadamu huambatana na maumivu au taabu, dhiki na magumu yanayopaswa yavumiliwe na, hatimaye, atafanikiwa. *Uchungu* katika methali hiyo hurejelea ugumu, mateso au taabu wakati wa kuhangaikia jambo fulani. Taabu hizo zinaweza kumfanya Mla akate tamaa na kushindwa kuyafikia malengo yake. *Utamu* huwakilisha mafanikio yanayopatikana baada ya kupata taabu au shida fulani. Kwa hiyo, 'mla cha uchungu na tamu hakosi' hurejelea kwamba, kila penye mahangaiko yenye kuambatana na taabu, shida au mateso, mafaniko yapo ndani yake. Kimsingi, methali hii hutia moyo, hufariji na kuhamasisha suala la uwajibikaji katika maisha halisi ya Waswahili. Hivyo, inapotumika hulenga kusisitiza kwamba hakuna kupata au kufanikiwa kiurahisi pasipo kufanya kazi kwa bidii. Waswahili humtazama mwajibikaji kama mtu anayevumilia taabu na changamoto mbalimbali katika mahangaiko yake. Kwa msingi huo, ndiye anayefaa katika ujenzi wa jamii, na yule mvivu anayependa kula pasipo jasho, anakwenda kinyume na kaida zao na huchukuliwa kuwa anakiuka maadili ya jamii kulingana na mgao wao wa majukumu (Oruka, 1990). Kwa kujiegemeza katika Nadharia ya Uhalisia kwamba fasihi ni akiso la maisha ya jamii, ni wazi kuwa mitazamo ya Waswahili kuhusu thamani na umuhimu wa uwajibikaji kupitia methali zinazomhusu Mla huakisi mazingira na kaida za maisha yao. Naye Kijogoo (2021) anaeleza kwamba kufanya kazi kwa bidii ni mbinu pekee inayopaswa kuzingatiwa na kila mtu ili kuongeza kipato kitakachodhihirisha thamani na uwepo wake katika jamii inayomzunguka. Hivyo, kupitia methali hii, Mla anapokumbana na taabu au mateso wakati wa kuwajibika kwake, hutafakari na kuvumilia akiamini kwamba ipo siku atafanikiwa.

Mchakato wa kuwajibika na kujituma kwa Mla unahitaji subira. Mla anasisitizwa kuwa na subira katika kila jambo analoliendea. Subira katika maisha ya Waswahili hutazamwa kama nguzo muhimu katika kuyafikia matarajio fulani. Pia, huhusishwa na uwezo wa kuvumilia changamoto zinazojitokeza katika safari ya kuyafikia matarajio hayo. Fasihi, hususani methali kama akiso la maisha ya jamii, hudokeza maadili yanayohusu umuhimu wa kuwa na subira kwa Mla. Mfano wa methali hizo ni "Mla mwenye pupa, hadiriki kula tamu".

Methali hii inasisitiza kwamba, Mla katika kuwajibika kwake lazima awe na subira. 'Mla mwenye pupa' katika methali hii ni kirai kinachorejelea mtu anayependa kufanikiwa katika jambo fulani kwa haraka. Vilevile, 'hadiriki kula tamu' humaanisha kwamba hawezi kufanikiwa katika kiwango anachokitarajia. Kwa mantiki hiyo, mla mwenye pupa hadiliki kula tamu humaanisha kuwamba mtu anayetaka kufanikiwa kwa haraka hawezi kuyafikia maono au matarajio yake. Hii ni kwa sababu anaweza kutumia njia ambazo si sahihi kulingana na utamaduni wake ili afanikiwe. Hatimaye, anaweza kufikwa na madhila fulani. Mathalani, anaweza kuiba au kudhulumu watu ili afanikiwe kwa haraka ambapo athari yake

anaweza kukamatwa na kufikishwa katika vyombo vya kisheria. Kwa kuongozwa na fikra za wanauhalisia, ni dhahiri kwamba kuwajibika pasipo kuwa na subira daima Mla hawezi kufanikiwa. Waswahili huamini kwamba mtu mwenye subira katika jambo lolote analolihangaikia, hufanikiwa kwa kiwango anachokitarajia. Maadili haya hurithishwa kizazi hadi kizazi kingine kupitia methali zao. Methali hii inapotumiwa katika mazingira halisi ya Waswahili hulenga kufunza maadili yanayohusu umuhimu wa kuwa na subira maishani. Subira hiyo itamwezesha Mla kutafakari kwa kina jambo analoliendea na kupata njia au mbinu mwafaka za kulifanikisha. Naye Calhoun (2018) anaeleza kwamba jambo lolote linapaswa kupewa muda wa kulitafakari ili kuondoa athari zitakazotokana na kutokuwa na maamuzi sahihi ya kuliendea jambo hilo. Hoja hii inathibitishwa vema na wahenga kama wasemavyo Subira yavuta heri au mvumilivu hula mbivu. Kwa jumla, methali za Kiswahili humsaidia Mla kukumbuka kwamba subira ni muhimu katika uwajibikaji wake.

### 4.5 Kutambua Athari za Kupokea Hisani

Hisani ni tabia ya kupenda kumtendea mema mtu (BAKITA, 2017). Kiuhalisi, Waswahili huheshimu na kuthamini hisani inayotolewa na mtu fulani. Wakati wa kupokea hisani huambatana na furaha zinazoonesha kuthaminiwa au kujaliwa na aliyetoa hisani hiyo. Athari ya kutendewa hisani hiyo huweza kubainika baadaye ambapo mpokezi huweza kufaidika au kupata zahama itakayogharimu maisha yake. Hivyo, katika kupokea huko, Waswahili humkumbusha Mla masuala kadhaa, yakiwamo yanayohusu namna ya kulipa hisani anayoipokea. Jambo hili hufanikishwa kupitia sanaa yao inayosukwa kwa kuakisi tamaduni zao. Mathalani, methali, “Mla mbuzi, hulipa ng’ombe” inadokeza maadili hayo.

Kula kitu kilichopokelewa kama hisani ni rahisi, lakini katika muktadha wa Waswahili ni deni linalopaswa kulipwa kwa ukubwa wake au maradufu. Methali hii inamkumbusha Mla kwamba kupokea ni rahisi kuliko kutoa, hivyo, akipokea hisani ndogo ya mtu fulani, atarajie kulipa hisani kubwa zaidi. Haya yanaelezwa zaidi na wahenga kwamba *hisani haiozi* na *ukipenda kupokea jifunze pia kutoa*. Kwa kuongozwa na fikra za wanauhalisia, sanaa ikiwemo, fasihi ni akiso la maisha ya jamii; suala hili linaonekana bayana katika mazingira halisi ya Waswahili ambapo katika shughuli za kitanzia na kiramsa watu hufanyiana hisani na urejeshaji wa hisani hizo huzingatia suala la ukubwa, ubora au wingi kulingana na kaida zao. Udokang (2014) anafafanua kwamba Waafrika huona fahari kulipa hisani kama mwendelezo wa mahusiano mema kwa kuzingatia misingi ya tamaduni za jamii husika. Vilevile, katika muktadha wa maisha ya Waswahili, methali hii inatumika kuonya tabia ya kudhulumu au kupenda kupewa vitu fulani na watu ambao lengo lao ni kutaka kupata malipo makubwa zaidi kutoka kwako au kitu kingine. Maishani mwao, huamini kwamba ni vizuri kutafakari na kutathmini kuhusu athari zitakazotokana na hisani hiyo kabla ya kupokea. Zaidi ya hayo, utoaji na upokeaji wa hisani kwa Waswahili maana yake kuzingatia tamaduni za

jamii husika. Kwa mfano, hisani ya mbuzi, ngòmbe, kuku, kanga na pombe maana yake hutegemeana na misingi ya utamaduni wa jamii. Hivyo, Mla hupokea na hutumia hisani husika akirejelea utamaduni wa jamii yake kuhusu maana ya hisani hiyo.

Methali ya ‘Mla mbuzi, hulipa ng’ombe’ inapotumika katika maisha halisi ya Waswahili huweza kuambatana na methali nyingine zenye kuundwa na neno mla ili kushadidia maudhui yanayolengwa kuwasilishwa. Mfano mmojawapo ni methali isemayo, “Mla cha mwenziwe, na chake huliwa”.

Methali hii hutumika kusisitiza maudhui yanayobebwa katika methali ya awali. ‘Mla cha mwenzake na chake huliwa’ huchochea maadili kwa Mla kwamba anapopokea au kukubali kula au kutumia kitu cha mtu mwingine, ametengeneza deni. Kwa msingi huo, awe tayari kutoa vitu vyake kwa ajili ya wenzake kama mwendelezo wa mahusiano ya kupeana. Jambo hili ni jema katika maisha halisi ya Waswahili na licha ya kusisitizwa katika mazungumzo ya kawaida, husisitizwa pia wakati wa shughuli za kiramsa na kitanzia. Mla hupewa angalizo kuwa daima awe makini na vitu anavyopatiwa na watu wengine. Vilevile, anaaswa kutafakari kwa kina kuhusu nia ya hisani inayotolewa kwake kabla hajaipokea. Naye Agozino (2018) anafafanua zaidi kwamba upokeaji na utoaji wa hisani kwa Waafrika ni masuala yanayobainisha heshima na upamoja katika maisha yao. Wakati mwingine, hisani au zawadi huweza kutolewa kama njia ya kuomba msamaha au kushukuru kwa kutendewa jambo fulani. Matokeo yanaonesha kwamba methali hii inamkumbusha Mla kuwa akipenda kutumia vitu vya wengine na vyake vitatumiwa kwa namna nyingine kwa kutaka ama la. Si lazima kiwe kitu cha aina ileile, kinaweza kuwa kingine na kikatumika kama malipo ya hisani aliyoipokea awali. Methali hizi zina tija kubwa katika maisha ya Waswahili kwa kuwa Mla ndiye anayeweza kunufaika au kuangamia kutokana na kupokea hisani kwa kujua au pasipo kujua. Kwa hiyo, anapoipokea lazima atafakari thamani ya hisani hizo na namna zitakavyorudishwa kulingana na utamaduni wa maana za hisani hizo. Kulingana na mtazamo wa wanauhalisia kwamba kazi ya sanaa isawiri ukweli wa maisha ya jamii, suala la kupokea hisani katika maisha ya Waswahili ni halisi na miongoni mwao hukumbwa na majanga kutokana na kupokea hisani hizo. Kwa hiyo, methali za Kiswahili zinasawiri ukweli wa maisha ya Waswahili wenyewe unaokitwa katika misingi ya maadili yao.

**4.6 Kutambua Athari za Wema na Ubaya**

Wema na ubaya ni masuala mawili kinzani kwa Waswahili. Katika maisha yao, huamini kwamba ubaya autendao Mla kwa wanaomzunguka, malipo yake humrudia mwenyewe kwa wakati asioutarajia. Hivyo, maishani mwao husisitiza maadili mema yanayobainika kwa vitendo avitendavyo Mla. Ili kuambukiza maadili hayo kwa jamii, hutumia fasihi yao, hususani methali zenye kuambatana

na neno ‘mla’. Mfano wa methali hizo ni “Mla kuku wa mwenziwe, miguu humwelekea”.

Kiuhalisi, katika maisha ya Waswahili, miguu ya kuku ni viungo visivyo na thamani ikilinganishwa na viungo vingine vya ndege huyo kama vile mapaja na kidali. Kwa kuzingatia kaida zao, kuku ni miongoni mwa ndege wenye thamani kubwa katika shughulli mbalimbali za kijamii na kitamaduni. Mathalani, inapotokea mgeni muhimu anafika nyumbani huandaliwa kuku kama kitoweo chenye thamani kwao. Katika maandalizi hayo, miguu huondelewa kwa kuwa haina thamani kulingana na tamaduni zao. ‘Mla kuku wa mwenziwe’ katika methali hii ni kifungu chenye kutumia lugha ya picha ambapo maana yake hutegemeana na malengo ya kutumika kwake. Kulingana na kaida za Waswahili kifungu hiki kinamrejelea mtenda maovu au msababishaji wa kutokea kwa jambo fulani baya kwa mwenzake. Pia, ‘miguu kumwelekea’ katika methali hii humaanisha kurudi kwa jambo fulani kwa mtenda au msababishaji wa jambo hilo. Matokeo yanaonesha kwamba methali hii inapotumika kwa Waswahili hulenga kusisitiza maarifa kuwa anayesababisha madhila au maumivu ya mtu fulani, maumivu yake humrudia yeye mwenyewe kama msababishaji. Hii ni kutokana na nguvu ya majonzi, dua na sala anazoomba kwa Mungu wake anayeaminiwa kuwa ni mwenye haki. Kumrudia kwa jambo hilo sio lazima liwe lilelile bali maumivu au uzito wake unaweza kulingana au ukazidi lile jambo alilomsababishia mwenzake. Waswahili huamini kwamba msababishaji wa jambo fulani baya lazima atavuna ubaya wake kabla hajafa. Hoja hii inafafanuliwa zaidi na Kijogoo (2021) kwamba maishani, ukimtendea ubaya mtu, nawe utavuna ubaya kama malipo ya ule ulioutenda. Kwa mantiki hiyo, methali hii inadhihirisha mtazamo wa Waswahili kwamba, katika kuishi, ni vema kutenda wema kwa kuwa malipo yake ni mema. Mtazamo huu unalandana na semi zao nyingi kama vile: *wema hauozi, mtenda mema huvuna mema* na *kazi mbaya si mchezo mwema* (Sumba, 2022). Methali hizi katika maisha ya Waswahili hutumika kama kuna viashiria vya Mla kumtendea maovu mwenzake ili abadili mwenendo huo. Kwa kuzingatia mawazo ya wanauhalisia yanayosisitiza kwamba sanaa hubainisha yale yaliyopo katika jamii, methali za Waswahili husawiri ukweli wa maisha yao. Hivyo, methali hutumika kama nguzo ya kuenzi na kuendeleza maadili ya jamii yanayohusu umuhimu wa kutenda wema na hasara za kutenda ubaya katika jamii yao.

Sambamba na hayo, Mla ndiye hutafuta ili aweze kula kulingana na utoshelevu wa mahitaji yake. Methali za Kiswahili zinabainisha maadili yanayohusu thamani na umuhimu wa Mla kula kwa njia halali. Kwa Waswahili, kutafuta riziki kwa njia halali ni maadili yanayoendelea kusisitizwa katika jamii kupitia sanaa zao. Mathalani, kuna methali zinazosisitiza kwamba anachopata Mla kwa halali ndiyo riziki yake halali. Kwa mantiki hiyo, kutafuta riziki kwa njia isiyo halali kunaweza kumsababishia matatizo katika maisha yake. Methali ifuatayo inabainisha maadili hayo “Mla kwa miwili, hana mwisho mwema”.

Methali hii hukemea tabia ya mwanadamu ya kutoridhika na akipatacho au alichonacho. 'Kula kwa miwili' ni kirai kinachobainisha ukweli wa utamaduni wa Mswahili katika uzingatizi wa kaida za mfumo mlo. Kwao, chakula huliwa kwa kutumia mkono mmoja, hususani wa kuume. Hivyo, kula chakula kwa kutumia mikono miwili ni kinyume na utamaduni wao. Methali hii inapotumika hulenga kusisitiza maadili ya kutochanganya njia au mbinu nzuri na mbaya au ovu katika kujipatia riziki. Kwa msingi huo, Mla anakumbushwa kwamba ili kujipatia mahitaji yake ya kila siku ni vema akazingatia misingi ya tamaduni za jamii yake inayokitwa katika uzingatizi wa njia halali. Kwao, Mla anayetumia njia zote mbili katika kujipatia mahitaji yake hana mwisho mwema na hawezi kufanikiwa. Njia ovu kwao, mathalani, kuiba, umalaya na unyangányi kwa ajili ya kupata kitu fulani, ni kinyume na utamaduni wao. Maarifa haya ya kimaadili humrejelea Mla kwa sababu ndiye anayeweza kutafuta riziki yake kwa njia hizo mbili na hata madhila yake humpata na kumwathiri yeye. Kutafuta kwa njia halali kwa Waswahili ni kitendo kinacholinda heshima na thamani ya Mla katika jamii yake. Haya yanaelezwa zaidi na Calhoun (2018) kwamba mwanadamu, maishani mwake, hutafuta ili aweze kustawi kwa kujikimu mahitaji yake na jamii kwa jumla. Anaendelea kueleza kwamba anayetafuta kwa njia zisizo halali daima huishia pabaya; hivyo, ni vema kutafuta kwa njia halali kulingana na misingi ya jamii husika. Kulingana na mtazamo wa wanauhalisia kwamba fasihi ni kielelezo halisi cha maisha ya jamii, Mla kula kwa miwili ni halisi katika maisha ya Waswahili. Kwa jumla, Mla anapaswa kuwa na subira katika kutafuta mlo ili isimkute hatari itakayoweza kumsababishia akose vyote. Hoja hii inayakinisha methali nyingine za Waswahili kama vile: kazi mbaya si mchezo mwema na mtaka yote kwa pupa hukosa yote.

**5.0 Hitimisho**

Makala haya yamejadili maadili mbalimbali yanayosisitizwa kwa Mla kupitia methali zilizohusisha neno mla kama msingi wa uundaji wa methali hizo. Matokeo yameonesha kwamba Mla anasisitizwa kuishi kulingana na maadili yanayozingatiwa na Waswahili wenyewe. Maadili hayo kupitia methali teule yanabainika kwa wapokezi kutokana na umilisi wao wa matumizi ya lugha kulingana na maana zinazowakilishwa. Kwa ujumla, methali zilizotafitiwa maana zake zinaweza kuwasilisha dhana zaidi ya moja kulingana na wakati na madhumuni ya kutumika kwake. Vipengele vya maarifa ya kimaadili vilivyojadiliwa ni pamoja na umuhimu wa kuwajibika katika maisha ya Waswahili ambapo Mla anapowajibika hupata heshima na familia yake kwa ujumla. Hivyo, asiyewajibika huchukuliwa kama asiyefaa katika ujenzi wa jamii yake na thamani yake hupungua ikilinganishwa na Mla mwajibikaji. Vilevile, imejadiliwa kuwa Mla asiyeridhika na alichonacho huweza kusukumwa kutenda maovu. Sambamba na hayo, Mla anasisitizwa kuwathamini na kuwajali ndugu zake kwani ndio watakaolia au kuhuzunika pamoja naye siku ya huzuni yake. Zaidi ya hayo, Mla

anakumbushwa kuzingatia maadili yanayohusu athari za kupokea au kutoa hisani kwa wanaomzunguka. Pia, suala la thamani ya wakati wa sasa kwa Waswahili limejadiliwa katika makala haya ambapo Waswahili huitazama leo kwa thamani zaidi kuliko jana na kesho isiyojulikana kwao. Pamoja na hayo, Mla anasisitizwa kutenda wema na kuacha mabaya katika jamii yake kwa kuwa kila akitendacho ni hazina katika maisha yake ya sasa na baadaye.

**Marejeleo**

Agozino, B. (2018) "The African Philosophy of Forgiveness and Abrahamic Traditions of Vengeance". *ARAS*, Juz. 39(2): 239-252.

BAKITA. (2017) *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers Ltd.

Bergner, R. (2010) "What is behavior? And so what?" *New Ideas in Psychology*, Juz. 28: 1-9.

Bertoncini, E.Z. (1989) *Outline of Swahili Literature: Prose, Fiction and Drama*. New York: Leiden Press.

Calhoun, C. (2018) *Doing Valuable Time: The Present, the Future, and Meaningful Living*. London: Oxford University Press.

Duwe, M. (2023) "Sifa za Hofu katika Maisha ya Mwanadamu: Uchunguzi wa Mhusika Ngoma

kutoka Riwaya ya *Ua la Faraja*". *Nuru ya Kiswahili*, Juz. 2(2): 74-102.

Duwe, M. (2024) "Epistemolojia ya Waafrika katika Semi Zilizoandikwa kwenye Vazi la Kanga za Waswahili". ***Journal of Kiswahili and Other African Languages***, Juz. 2(2): 14-24.

Gencer, H. (2019) "Group Dynamics and Behaviour". *Universal Journal of Educational Research*, 7(1): 223-229. Inapatikana katika https://www.researchgate.net/publication /331482821. Ilisomwa tarehe 18 Juni 2024.

Hart, K. (2019) *Money is How We Learn to be Human*. London: University of London.

Kamugisha, F.M. (2020) *Maisha ni Mtihani: Ukibadili Maana ya Maisha Unabadili Maisha Yako*. Dar es Salaam: Eternal Word and Charity Publishing (EWCP).

Kijogoo, S.D. (2021) *Saikolojia na Maisha: Ishinde Hofu, Boresha Maisha yako, Chagua Marafiki, Tunza Muda*. King Kijogoo Publishers.

Larkin, M. (1977) *Man and Society in the Nineteenth Century Realism: Determinism and Literature*. London: Macmillan Press.

Madumulla, J.S. (2009) *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia, na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Limited.

Mbiti, J.S. (2011) *African Religions and Philosophy*. Kampala: East African Educational Publishers.

Miruka, O. (2005) *Incounter with Oral Literature*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mlaga, W.K. (2017) *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi: Karne ya 21*. Dar es Salaam: Heko Publishers.

M'Ngaruthi, T.K. (2008) *Fasihi Simulizi na Utamaduni*: Nairobi: Jomo Kenyata Foundation.

Mulokozi, M.M. (2017) *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: KAUTTU Limited.

Ogechi, N.O. (2024) *Taratibu za Kuendesha Utafiti na Masuala Mengine*. Kenya: The Jomo Kenyatta Foundation.

Okpewho, I. (1992) *African Oral Literature*: USA: Indiana University Press.

Prior, A.N. (1967) *Past, Present and Future.* USA: Oxford University Press.

Sengo, T.S.Y na Kiango, S.D. (1973) *Hisi Zetu*. Dar es Salaam: TUKI.

Senkoro, F.E.M.K. (1988) *Ushairi, Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: DUP.

Simiyu, W.F. (2011) *Kitovu cha Fasihi Simulizi: kwa Shule, Vyuo na Ndaki*. Mwanza: Serengeti Bookshop.

Sumba, T.O. (2022) *Dira ya Methali: Kitabu cha Marejeleo*. Nairobi: African Ink Publishers.

Udokang, E. J. (2014) "Traditional Ethics and Social Order: A Study in African Philosophy".Cross-Cultural Communication, Juz. 10(6): 266-270. Inapatikana katika https://core.ac.uk/download/pdf/236298825.pdf. Ilisomwa tarehe 16 Julai 2024.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Wamitila, K.W. (2018) *Kamusi ya Methali*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Westphal, K.R. (1989) *Hegel's Epistemological Realism: A Study of the Aim and Method of Hegel's Phenomenology of Spirit*. Dordrecht: Kluwer Academic Publisher.

Widmer, E. (2006) "Who Are My Family Members? Bridging and Binding Social Capital in Family Configurations". *Journal of Social and Personal Relationships*, Juz. 23: 979-998. Inapatikana katika https://doi.org/10.1177/0265407506070482. Ilisomwa tarehe 18 Juni 2024.